TANGAZO LA SERIKALI NA. 335 la tarehe 17/6/2022

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16 (1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA KITUO CHA MAGARI) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA, 2022

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Kituo cha Magari) (Marekebisho) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka 2022, na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Ushuru wa Kituo cha Magari) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka, 2020 ambazo zitajulikana kama Sheria Ndogo Kuu na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Marekebisho GN Na. 833 ya tarehe 2/10/2020

2. Marekebisho yamefanyika katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo Kuu kwa kufuta ushuru wa shilingi 1500 kwa bajaji na badala yake kuweka ushuru wa shilingi 500 kwa bajaji.

Lakiri ya Halmashauri imegongwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika mkutano mkuu wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Mbeya uliofanyika mnamo tarehe…………Mwezi …………., 2022 na lakiri iliyogongwa na kushuhudiwa na:-

TRIPHONIA KISIGA,
*Kaimu Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Jiji la Mbeya*

DORMOHAMED ISSA RAHMAT,
*Meya*
*Halmashauri ya Jiji la Mbeya*

NAKUBALI,

**L.S**

INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (MB)
*Waziri wa Nchi-Or-Tamisemi*